



## Msikae juu ya makaburi, na wala msisali kwa kuyaelekea

Imepokewa Kutoka kwa Abuu Marthad Al-Anawiy -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Msikae juu ya makaburi, na wala msisali kwa kuyaelekea".

[Sahihi] [Imepokelewa na Imamu Muslim]

Amekataza -Rehema na amani ziwe juu yake- kukaa juu ya makaburi. Kama alivyokataza kusali kwa kuyaelekea makaburi, kwa kaburi kuwa upande wa kibla cha mwenye kusali; kwa sababu hilo ni katika njia za shirki.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/10647>

النجاة الخيرية  
ALNAJAT CHARITY

